



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na.KDC/L.50/9/VOL.I/40

Tarehe: 05/09/2022

Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S.L.P 2320,  
KONDOA.

**YAH: KUWASILISHA TANGAZO LA MARUDIO LA NAFASI MBILI (02) ZA KAZI**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Nawasilisha tangazo la marudio la nafasi mbili (02) za kazi za Kada ya Katibu Mahsusi Daraja la III ambazo hazikujazwa baada ya kufanya usaili tarehe 30 – 31/08/2022 kwa sababu hatukupata wasailiwa waliokidhi sifa za kuajiriwa.

Kwa barua hii, nawasilisha tangazo la marudio Kumb. Na. KDC/L.50/9/VOL.1/39 la tarehe 05/09/2022 ili uweze kutangaza nafasi hizo kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira.

Natanguliza shukrani.



Mashauri M. Vicent

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KONDOA**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KONDOA**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KDC/L.50/9VOL.I/39

Tarehe 05/09/2022

**YAH: TANGAZO LA MARUDIO YA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

**1. KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III – NAFASI 2**

**Sifa:**

- Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu Kidato cha Nne (IV)
- Awe na cheti cha mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu
- Awe amefaulu somo la Hatimkato na Shorthand maneno 80 kwa dakika moja
- Awe na mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows Microsoft word, Excel, Publisher. Internet na E-mail.


**MAJUKUMU**

- i. Kuchapa barua
- ii. Kusaidia kupokea wageni, kuwasikiliza shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anayofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao
- vi. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi

## MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe rala wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa
2. Mwombaji awe na umri kati ya mlaka 18 na usiozidi 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela
3. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Details CV) namba za simu na anwani sahihi
4. Maombi yote ya mwombaji yaambatane na nakala za Vyeti vya Taaluma, vyeti vya kidati cha (IV au VI), Cheti cha kuzaliwa na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
5. Testimonials na "Provisional statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NACTE) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi
7. Siku ya Usaili kila mwombaji afique na Vyeti halisi (Original) vya Elimu, Taaluma, Kuzaliwa na Kitambusho.
8. Waombaji waliostaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
9. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
10. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18 Septemba, 2022.
11. Maombi yaambatanishwe na Nakala ya kitambulisho cha NIDA au namba ya kuandikishwa.
12. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anwani ya:-

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa,  
S.L.P 01,  
KONDOA.**

  
Mashauri M. Vicent  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KONDOA**  
**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KONDOA**